JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
MKOA WA RUKWA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

SHULE YA SEKONDARI KIRANDO
S.L.P 107
NAMANYERE-NKASI
TAREHE 28/03/2022.

NAMBA ZA SIMU.

MKUU WA SHULE

0754 530 654
0623 975 951
0737 951 172

MATRONI

0763 417 567

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI_____.
S.L.P_____,_____

YAH :MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIRANDO
HALMASHAURI YA NKASI MKOA WA RUKWA
KIDATO CHA TANO JULAI MWAKA 2022.

1.Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2022 Tahasusi ya _____shule hii ipo umbali wa km 60 kutoka mji wa Namanyere,usafiri kutoka Sumbawanga mjini unapatikana, panda gari za moja kwa moja kuja Kirando na kwa wanaotokea Mpanda panda gari za Sumbawanga, ukifika Namanyere shuka halafu panda gari za Kirando.

Muhula wa masomo utaanza tarehe itayotangazwa na wizara , Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyotangazwa na mwisho wa kuripoti ndani ya siku 14 toka tarehe ya kuripoti kama tangazo la serikali lilivyotangazwa,

Kuchelewa kuripoti kutampotezea nafasi .

2.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 ADA NA MICHANGO YA SHULE

a. Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= Lipa nusu yaani **35,000/=**
b. Fedha ya ukarabati wa samani za shule ni shilingi **15,000/=**
c. Kitambulisho na picha **6,000/=**
d. Fedha kwa ajili ya taaluma ni shilingi **20,000/=** kwa mwaka.

Scanned with CamScanner

e. Fedha kwa ajili ya kuwalipa wapishi ,walinzi,na vibarua wengine ni shilingi **30,000/=**
f. Fedha ya huduma ya kwanza (matibabu) ni shilingi **10,000/=,**
ANGALIZO: mzazi/mlezi ni vizuri kumpa mwanao fedha ya kutosha kwa ajili ya matibabu.Na kama ana bima ya NHIF aje nayo.
g. Nembo ya shule shilingi **2000/=**
h. Huduma ya umeme shilingi **5,000/=**
i. Fedha ya tahadhari shilingi **5000/=.**

Jumla ya fedha kwa hapa ni **Tsh 128,000/= (Muhimu** ada ni nusu muhula).

ANGALIZO:

Wawapo kidato cha sita kutakuwa na michango ya mitihani ya mkoa ,Joint na taifa,mtajulishwa kwa wakati husika ufikapo.

Fedha hii na nyinginezo ziwekwe katika akaunti ya shule .
Jina la akaunt **DEVELOPMENT KIRANDO SECONDARY SCHOOL**
A/C 62001100059 BENK NMB.
Ajapo aje na Pay in slip ya benk.

2.2.SARE ZA SHULE.

A. Sketi 2 (mbili) kwa wasichana rangi ya brue bahari mpauko na nyeusi ikiwa na tai mbili nyeusi na blue bahari *(Mshono linda box malinda 3 madogo pembeni kila upande ,kubwa moja nyuma na mbele.*
ANGALIZO:*Sketi iwe ndefu hadi karibu na kifundo cha mguu angalia picha ,ukishona sketi fupi utarudia tena.*
B. T-shirt rangi ya bluu (muundo form six) yenye kola nyeupe.
C. Nguo za kushindia shamba dress rangi damu ya mzee drafuti ndogo mshonee (mshono solo picha imeambatanishwa na fomu hii.
D. Viatu vya shule ni vyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi.
E. Sare za michezo ni truick suit rangi ya bruu bahari ,viatu raba nunua mwenyewe.
F. Soksi jozi mbili nyeupe,nunua
G. Sweta rangi ya brue bahari ,nunua mwenyewe ila si lazima sana kuna joto.
H. Rangi ya hijab kwa waislamu ni nyeupe isiwe ndefu kupita kiasi.
I. Mashati mawili mikono mirefu hayo nunua mwenyewe hukohuko.

2.3 MAHITAJI MENGINE,

a) Ream moja ya karatasi kwa kila muhula.
b) Vitabu vya masomo ya tahasusi aliyopangiwa ili kumsaidia usomaji.
c) Scientific calculator kwa wanaosoma Jiografia.
d) Godoro la kiwanafunzi futi 2.5
e) Mashuka mawili rangi ya pink.pia shuka zito au blanketi nyepesi.
f) Chandarua moja kujikinga na mbu.
g) Vyombo vya chakula sahani,kikombe,kijiko na bakuli.
h) Ndoo mbili ndogo kwa matumizi yake.
i) Vifaa vya usafi (a) kwanja 1,(b) jembe 1,(c) reki 1 na fagio ya kufagilia.

Scanned with CamScanner

3.SHERIA ZA SHULE :

MAKOSA YANAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- Wizi
- Kutohudhuria masomo kwa siku 90 bila taarifa.
- Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa walimu/wanafunzi/walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika kwani wanafunzi kwa hapawakuwa na nywele fupi.
- Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati,uhusiano wa jinsi moja,kuoa au kuolewa.
- Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- Kushiriki matendo ya uhalifu ,siasa,na mengineyo yanayovunja sheria za nchi.
- Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau bendera ya Taifa.
- Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

MUHIMU: Soma kwa makini maelekezo yaliyotolewa.,pia hatuna chakula maalumu (special diet).

KARIBU SANA .



Scanned with CamScanner

SHULE YA SEKONDARI KIRANDO

FOMU YA KUKIRI KUKUBALI SHERIA ZA SHULE.

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI.
JINA LA MWANAFUNZI----------

KIAPO CHA UTII:

MIMI----------
Nikiwa mwanafunzi wa Shule hii na kubali kuwa,umma wa nchi hii yaTanzania Ndiyo ulionipa nafasi hii maalum ya masomo,ili nimalizapo niweze kulitumikiaTaifa Na kuleta Maendeleo.

Hivyo basi,ninaahidi kwamba,nitajibidisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule.Ili Kutimiza shabaha hiyo ,ninakubali nakuahidi kwa hiari yangu mwenyewe kuwa Nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa na walimu wangu.Nikiwa na Malalamiko au maoni nitayafikisha kwa viongozi wa shule kufuatana na utaratibu Uliowekwa bila ya kuongeza chochote. Nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua za Kinidhamu zinazostahili iwapo nitakuwa nimekiuka sheria za shule.

Sahihi ya mwanafunzi----------tarehe----------

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ---------- ambaye ni mzazi/mlezi wa Mwanafunzi mtajwa hapo juu,naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule Katika kumlea mwanangu.Hii ikiwa ni pamoja na kutomruhusu mwanangu kuja na Simu shuleni. Nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba nitakuwa tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa kwa mjibu wa sheria na kanuni za shule iwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.

Sahihi ya mzazi/mlezi ----------
Namba ya simu ya mzazi/mlezi----------
Tarehe:----------
Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Scanned with CamScanner

KIRANDO SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 107,
NAMANYERE-NKASI.

MEDICAL OFFICER,

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine the above named as to His/Her fitness to is/her fitness as indicated below.Arrange for necessary treatment so that the certificate may besigned and brought to school by the student.
This certificate must be signed by aqualified Medical Officer of recognized hospital.

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named student with regard to:

Skin:---------- Abdomen:----------
Eyes:---------- Urine:----------
Teeth:---------- Hemoglobin:----------
Spleen:---------- Chest:----------
Anydisabilities:----------

I Consider that:----------He/She is in good health Free from infections diseases,and fit to come to school, He/She is fit to come to school after having:----------Treatment for:----------
----
----------She is not pregnant.

MEDICAL OFFICER SIGN _____ STAMP_____

DATE.....

Scanned with CamScanner

RANGI NA MSHONO WA SARE ZA SHULE KATIKA PICHA

Hii ni blue bahari mpauko ,shona kama uonavyo picha.

Scanned with CamScanner

HII SKETI NYEUSI

finix HOT 10

Scanned with CamScanner



HII NI DAMU YA MZEE DRAFTI NDOGO

MUHIMU:

Kama kuna sehemu hujaelewa uliza usaidiwe,

0754530654 / 0737951172 / 0623975951 MKUU WA SHULE.

Infinix HOT 10

Scanned with CamScanner